

INJILI ISIYOBADILIKI KATIKA ULIMWENGU UBADILIKAO

Twaishi katika zama za mabadiliko. Fikiria njia za usafiri ukilinganisha na miaka 50 iliyopita. Angalia njia za kujipatia vipato ukilinganisha na miaka 50 iliyopita, na hatuwezi kujiepusha zaidi ya kuona mabadiliko mengi yaliyotokea. Kwa mujibu wa teknolojia, inasemekana kwamba katika miaka 50 hadi 60 iliyopita tumebadilika zaidi kuliko tulivyokuwa katika miaka 500 iliyotangulia. Baadhi ya mabadiliko ni mazuri na mengine siyo mazuri kutegemeana na kilichobadilika.

Tukijiangalia, twaona kuwa wengine wangebadili injili. Wengine wanadhani kuwa injili haimtoshelezi mwanadamu wa sasa. Tatizo ni kwamba mwanadamu hataki kuishi katika viwango vya neno la Mungu. Kwa miaka na miaka, asili ya mwanadamu haijabadilika. Walakini wanadamu wamebadili injili (Marko 7:7, 8). Injili iliyobadilishwa, Mtume Paulo alisema ni injili iliyogeuzwa (Wagalatia 1:6, 7).

Tunapoyatafakari mahitaji ya kibinadamu, twaona ya kwamba mahitaji yaliyo mengi hayajabadi. Mathalani, wokovu ulihihitajika baada ya anguko bustanini (Mwanzo 3), na hadi leo mwanadamu angali anahitaji wokovu (Warumi 3:23; 6:23). Ili wokovu upatikane, kwa kuheshimu haja hii, ni lazima tuwe na injili isiyobadilika katika uliwengu ubadilikao, na ndiyo tunayotaka kuizingatia kwenye makala hii.

SABABU ZINAZOIFANYA INJILI ISIBADILIKE

Mabadiliko yamekatazwa (Wagalatia 1:6-9; Warumi 1:16, 17). Ukweli ni kwamba, maandiko yamewezeshwa kikamilifu kutupatia mambo ya lazima kwa wokovu (2 Timotheo 3:16, 17; 2 Petro 1:3). Hayo ndiyo mambo yaliyowaokoa watu siku ya Pentekosti (Matendo 2:37-41), Wakorintho (1 Wakorintho 15:1, 2) na yatamwokoa kila mwamini mtiifu (Marko 16:15, 16; Waebraania 5:9).

Injili ni uweza unaobadilisha ufedhuli wa mwenye dhambi ili awe mtu mtakatifu. Ilimbadilisha Sauli, ambaye, yeeye mwenyewe alijiona kwamba ni mwenye dhambi wa wenyе dhambi (1 Timotheo 1:15). Ilibadili maisha ya Wakorintho (1 Wakorintho 6:9-11). Hata leo, ina uweza ule ule wa kumwokoa Yule atafutaye wokovu (Mathayo 11:28-30; Warumi 1:16).

Tunapoifikiria dhambi, twaona kuwa haijabadilika na haitabadilika (Yakobo 1:13-15). Njia moja moja za majoribu zinaweza kubadilika. Walakini, dhambi hutokea kwa kutumia kati ya njia hizi;

Tamaa ya mwili.

Tamaa ya macho.

Kiburi cha uzima – Mathayo 4:3-11; 1 Yohana 2:16.

Injili ilitolewa mara moja kwa wote (Yuda 3) ili kuondoa hizi dhambi.

MTU ANAWEZAJE KUHUBIRI INJILI ISIYOBADILIKI

Kwanza ,tunatakiwa kuhubiri mamlaka ya Kristo (Mathayo 28:18-20).Pili, Tunatakiwa kuhubiri kuhusu kanisa ambalo Yesu aliahidi na alilijenga, ambapo ndani yake wokovu unapatikana (Mathayo 16:18; Matendo 2:47).

Tatu, tunatakiwa kuhubiri kuhusu vigezo vya injili vya wokovu.

Kusadiki kuwa Yesu ndiye Kristo - Yohana 8:24

Kutubia Dhambi - Matendo 2:38; 17:30

Kukiri imani katika Kristo - Mathayo 10:32, 33;

Warumi 10:10

Kubatizwa katika Kristo kwa ondoleo la dhambi - Mark

Marko 16:16 Acts 2:38; 1 Peter 3:21

Nne, tunatakiwa kuhubiri kuhusu umoja wa Roho ili kuleta “kifungo cha amani” (Waefeso 4:3). Yesu aliomba kwa ajili ya huu umoja baina ya waaminio wa wakati ule na sasa (Yohana 17:20-21). Katika kanisa lililokuwepo Korintho Mtume Paulo alisihi sana kwa ajili ya umoja (1Wakorintho 1:10). Mungu ametoa utaratibu wa umoja katika Neno lake (Waefeso 4:1-6)

HTIMISHO

Ingawa tunaishi katika zama za mabadiliko, kamwe tusiibadili injili ya Kristo.

Wanadamu wamejaribu na kushindwa. Uweza wa injili umebaki vilevile kama

ilivyokuwa katika karne ya kwanza. Kwa kujua kwamba Mungu atatulaani endapo tutaibadili, je ndiyo tusiikubali, tusiiamini, tusiitii na kuihubiri? (Wathesalonike 2:13)